



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UCHUKUZI
**SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA
TASAC**



IMETHIBITISHWA ISO 9001:2015

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU HATUA ZILIZOCHUKULIWA KWA MELI YA MV. WANKYO

Dar es Salaam, 17 Desemba, 2023

Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) limeona taarifa inayosambaa kwenye mitandao ya kijamii kuhusu tukio la Meli ya MV. Wankyo kuigonga Meli ya MV. Kyone mnamo tarehe 08 Desemba, 2023 majira ya 10:25 jioni, jijini Mwanza wakati ikitokea Bandari ya Bukoba kuelekea bandari ndogo ya Igogo iliyoko Mwanza Kusini (Mwanza South).

Kufuatia taarifa hizo, TASAC imefanya uchuguzi wa awali ambapo imethibitisha kutokea kwa tukio hilo na tayari hatua za awali za kisheria zimeanza kuchukuliwa kwa meli ya MV.Wankyo ikiwemo;

- i. Kuwasiliana na Mmiliki wa meli ili kupata taarifa rasmi kuhusu tukio hilo;
- ii. Kumsimamisha nahodha wa meli ya MV. Wankyo kuendelea kutoa huduma kama nahodha mpaka uchunguzi utakapo kamilika; na
- iii. Kuzifanyia ukaguzi meli zote mbili ambapo ukaguzi kwa Meli ya MV.Wankyo ili kujua uwezo wa utendaji kazi katika mifumo ya meli ikiwemo mfumo wa kuongozea na Meli ya MV.Kyone ili kubaini iwapo imepata athari zozote.

TASAC inaendelea na uchunguzi wa kina kuhusu tukio hilo na itatoa taarifa kwa umma mara baada ya kukamilika kwa uchunguzi huo.

Aidha, TASAC inatoa wito kwa wadau wote wa usafiri majini kuhakikisha wanazingatia taratibu za usalama zilizowekwa katika uendeshaji wa vyombo vya usafiri majini ili kuepusha madhara yanayoweza kutokea kwa binadamu, mizigo, meli pamoja na uharibifu wa mazingira ya majini.

**Imetolewa na;
Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu,
Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC)
17 Desemba,2023**